

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI MANISPAA YA KINONDONI ROBO YA TATU

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leo Alhamisi tarehe 17/05/2018 katika Mkutano wake wa kawaida wa Baraza robo ya tatu uliofanyika katika ukumbi wa Manispaa, pamoja na mambo mengine limepitia na kupitisha taarifa mbali mbali za utekelezaji wa kazi za kamati tano za kudumu na taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Robo ya tatu na ambapo zaidi ya maazimio na 12 kutoka kamati hizo na taarifa zilizopitiwa yameridhiwa..

Kutoka Kamati ya Huduma za Uchumi Afya na Elimu chini ya Mhe.Thadey S. Masawe yenye jukumu la kutoa huduma za kijamia kwa wakazi wa Kinondoni maazimio matano yamewasilishwa na kupitishwa kutoka katika sekta zinazohusu kamati hiyo kama ifuatavyo :-

- Kuitaka Idara ya Mipangomiji kwenda kujiridhisha kuhusiana na mgogoro wa uvamizi katika eneo la Sekondari ya Salasala ili kujua idadi ya watu wanaotakiwa kufidiwa na kiasi cha fedha kinachohitajika kulipa fidia ili kuruhusu upanuzi wa Shule hiyo.
- Imeitaka Idara ya Mipangomiji Kitengo cha Upimaji kwenda kujiridhisha kuhusiana na mipaka na umiliki wa eneo la Soko la Mbezi beach ili kuruhusu kuanza kutumika.
- Waheshimiwa Madiwani wote kupewa Free pass kuishangilia Timu ya Manispaa ya Kinondoni kila itakapocheza katika uwanja wa nyumbani ili kuongeza hamasa kwa Timu.
- Afisa Elimu wa Sekondari atembelee Sekondari ya Kata ya Mikocheni na kuzungumza na Kamati ya Maendeleo ya Kata hiyo kuhusiana na changamoto zilizopo katika shule hiyo na namna bora ya kuzipatia ufumbuzi.
- Wajumbe wa Kamati husika wapewe vyanzo vya mapato vinavyohusiana na kamati husika ili waweze kuweka mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato hayo sambamba na kuundwa kikosi kazi cha kufuatilia ukusanyaji wa Mapato.

Kamati ya Mipangomiji na Mazingira chini Mhe.Songoro Mnyonge yenye jukumu la kusimamia upangaji na uendelezaji wa mji ndani ya manispaa imewasilisha maazimio mawili kama ifuatavyo:-

- Kuandika barua kwa Mamlaka zilizozuia uondoshaji wa mchanga katika mito ili ziruhusu kuondolewa ili kukabiliana na Mafuriko katika kipindi hiki cha mvua kwani mito mingi

imejaa michanga inayozua maji kupita katika njia yake. Aidha Wah. Madiwani wajengewe uelewa katika suala la usimamizi wa Mito hiyo.

- TARURA iombwe kutenga fedha kwa Matengenezo ya barabara kwa dharura kutokana na barabara nyingi kuharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Kamati ya Maadili ya Manispaa chini ya Mhe. Tatu Malyaga ilikuwa na mazimio mawili la kuwataka Wajumbe wa vikao kuzingatia muda wa vikao na ziara ili kuanza na kumaliza kwa wakati na suala zima la kutoa elimu zaidi kwa Wah. Madiwani na Watumishi namna ya kuwasilisha Malalamiko katika Kamati husika.

Kamati ya kudhibiti UKIMWI chini ya Naibu Meya Mhe, George Manyama imetoa maazimio matatu:-

- Kumtaka mratibu wa Kitengo cha ukimwi kufuatilia katika shule zote ili kupata mrejesho kuhusiana na mwitikio wa Wazazi wa Wanafunzi katika suala zima la kupima afya.
- Wakuu wote wa Shule za msingi na Sekondari kwa kushirikiana na Wakaguzi wa Elimu wafuatilie ufundishaji wa elimu ya dini mashuleni ili ipewe uzito unaostahili kama masomo mengine.
- Mchumi wa Manispaa afuatilie matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mafunzo ya Wah. Madiwani ili zitumike kwa wakati kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya UKIMWI.

Kamati ya Fedha na Uongozi chini ya Mstahiki Meya Mhe. Benjamini Kawe Sitta yenye jukumu la kusimamia masuala yote ya fedha na utawala wa Manispaa imewasilisha maazimio mawili:-

- Watendaji wote walioweza kupatikana kwa hati safi kutokana na Ripoti ya Mdhibiti na mkaguzi wa Hesaba za Serikali watambuliwe kwa kupewa zawadi kama Motisha kwa kuiletea Manispaa Hati safi.
- Manispaa iangalie uwezekano wa kuongeza nguvu katika kushughulikia mgogoro wa Cocobeach ili Mapato yanayotakiwa kukusanywa yapatikane. Mwisho, pamoja na Maazio hayo wah. Madiwani walipitisha mapato na matumizi ya Manispaa robo ya tatu na taarifa nyingine sambamba na kupata majibu na ufafanuzi wa Masuala kutoka Sekta mbalimbali kupitia Maswali ya Papo kwa Papo yaliyojibiwa na kufafanuliwa kwa ufasaha na Mkurugenzi Wa Manispaa ya Kinondoni Ndugu Aron T. Kagurumjuli kama Sheria na kanuni zinavyotaka.

IMETOLEWA NA:-

**Sebastian M. Mhowera**  
**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA.**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**